

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
ISO 9001:2015 CERTIFIED



TAARIFA KWA UMMA

SHINDANO LA WASICHANA KATIKA TEHAMA (AI HACKATHON) 2026

Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICTC) inawaalika wanafunzi wasichana wanaosoma vyuo vikuu nchini, kushiriki katika mafunzo na shindano la Wasichana katika Akili Mnemba (**Girls in ICT – AI Hackathon**) 2026.

Shindano hili linalenga kuunda mawazo na dhana bunifu zaidi zinazohusiana na kaulimbiu ya maadhimisho ya Wasichana katika TEHAMA mwaka 2026 isemayo: **“AI for Development: Girls Shaping the Digital Future”**.

Shindano hili ni jukwaa la kipekee kwa wasichana kushiriki kikamilifu, kuonesha ujuzi wao na kufurahia ubunifu, uvumbuzi na ufanisi na hatimaye kufuzu kutengeneza suluhisho za kiteknolojia kwa ajili ya kutatua changamoto za jamii.

Taarifa za Shindano

| | |
|--------------------------------|---|
| Tarehe za Shindano | 23 – 27 Machi, 2026 |
| Mahali | Arusha |
| Vigezo | <ol style="list-style-type: none">Mwanafunzi wa kike Mtanzania anayesoma katika Chuo Kikuu nchini;Ujuzi wa msingi wa lugha za programu (Mfano Python na R);Umri kuanzia miaka 18 hadi 24;Uanachama katika Klabu ya Kidijiti ni sifa ya ziada itakayopewa kipaumbele. |
| Kiunganishi cha Usajili | https://digitalclubs.tz/GICT2026 |
| Mwisho wa Usajili | 15 Machi, 2026 |
| Zawadi na Motisha | <ol style="list-style-type: none">Zawadi kwa kundi litakaloshinda;Vyeti kwa washiriki wote;Utambuzi maalum katika siku ya maadhimisho. |

Washiriki watakoachaguliwa watagharamikiwa malazi, chakula pamoja na usafiri katika kipindi chote cha shindano.

Wanafunzi wote wa kike wenye vigezo vilivyotajwa, mnahimizwa kujisajili kupitia kiunganishi hapo juu kwani nafasi ni chache hivyo ni muhimu kuwahi.

Imetolewa tarehe **6 Machi 2026**.

Dkt. Jabiri K. Bakari
MKURUGENZI MKUU